



## Maswali na Majibu(Vijana)

### Q. Kwanini vijana wanawekwa kwa makini?

Kila siku watu elfu kumi na nne wanaambukizwa virusi vya ukimwi na asilimia hamsini ya watu hawa ni vijana kwasababu hii vijana wanaangaliwa n akupewa umakini spesheli wakati wa kuwaeleza kuhusu ugonjwa wa ukimwi ,asilimia sitini ya vijana hawa ni wasichana.

### Q. Kwanini vijana wanaambukizwa kwa hali ya juu?

Hakuna jibu rahisi kwa swali hii kwani kuna sababu mingi.Kwanza ni vijana wanaanza kuelewa miili zao na wanaanza kufanya mapenzi bila ya kujua hatari ya kuambukizwa virusi vya ukimwi, pili ni umakini kwani umasikini unawafanya wafanye vitu ambazo kama wangeweza kujikimu kimaisha hawangefanya . Wasichana wadogo wanataka pesa ama wanataka kulipa karo na hii inawafanya wafanye mapenzi na wazee ili wapate pesa ,wazee hutafuta wasichana wadogo ili wafanye mapenzi nao na baadaye wawalipe.Pia nchi zingine wasichana wanabakwa na hii inaongeza nambari ya wasichana wanaoambukizwa virusi , pia televisheni inaonesha ni sawa kuwa na zaidi ya mpenzi mmoja.

### Q. Majumuiya(makampuni) zinafanya kazi na watu waliokomaa ,tufanye nini?

Vijana wanaweza badilisha mwenendo wa kisasa na kusaidia siku zijazo. Utafiti unaonesha yakwamba vijana wanaweza badilisha tabia zao wakilinganishwa na watu wengine wakifundishwa juu ya virusi vya ukimwi.Pia vijana wanaweza chukua jukumu na kufundisha wenzao kwa mfano **Working to Empower** huwa na vikundi vya vijana ambao wameungana kubadilisha jamii zao.Kila wiki wao hukutana na kufundishana juu ya ugonjwa wa ukimwi.Katika kambi moja ya wakimbizi vijana hawa wameweza kuongeza nambari ya watu wanaopimwa virusi vya ukimwi kwa asilimia hamsini kila mwezi kutoka wakati **working to Empower** iliawafundisha kuhusu virusi vya ukimwi.

### Q.Kama siko kwa **Working to Empower** ama jumuiya yeyote ,napaswa kufanya nini?

Wakati **Working to Empower** ilikuwa inafanya kazi huko Benin , kijana mmoja alisikiza semina ambayo ilikuwa inaendelea na akaamua kufanya kitu kuhusu virusi vya ukimwi alichukuwa makaratasi ya semina hiyo ambayo yalikuwa yanahusu virusi vya ukimwi na kuuliza marafiki wake wamsaidie ,na akaenda shule yake na kufundisha wenzake kuhusu ugonjwa wa ukimwi.Hii ni mfano yakuonesha vile kijana huyu aliamuwa kubadilisha jamii yake bila kuambiwa na mtu yeyote.